# JARIDA MAALUM

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

www.mwt.go.tz | Toleo la Agosti, 2022 | Tanzania



**Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, Akikagua Hatua za Ujenzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II), Awamu ya Pili Unaoanzia Eneo la Mbagala Hadi Gerezani Ambao Umefikia Asilimia 66.6 na Unatarajiwa Kukamilika Ifikapo Mwezi Februari, 2023.**



#UtekelezajiWUU2022

# Prof. Mbarawa Abainisha Vipaumbele Ujenzi wa Miundombinu

Na **Segolena Francis -** WUU

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amesema vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/23 vinakusudia kuhuisha uchumi wa nchi na kuwakomboa Watanzania wa ngazi zote.

Akizungumza jijini Dar es Salaam leo, Prof. Mbarawa amevitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kukamilisha ujenzi wa barabara za lami zinazounganisha mikoa yote nchini ili kurahisisha huduma za usafiri na uchukuzi katika sekta mtambuka.

Amevitaja vipaumbele vingine kuwa ni ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi lenye urefu wa km 3.2 Jijini Mwanza, kukamilisha Daraja la Wami linalounganisha Mkoa wa Pwani na Tanga, na Ujenzi wa Barabara za kupunguza msongamano na magari yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam na Barabara za mzunguko jijini Dodoma.



**Prof. Makame Mbarawa**
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*

Ameeleza kuwa Serikali pia itaendelea na upanuzi wa Bandari za Dar es Salaam na Tanga, Ujenzi wa Meli katika Ziwa Victoria na Tanganyika, upanuzi wa viwanja vya ndege nchini na ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi wa umma katika maeneo mbalimbali nchini.

***"Tumejipanga kuhakikisha miradi hii tunayoitekeleza inazingatia thamani ya fedha na kuzalisha ajira kwa Watanzania wenzetu kadri inavyowezekana,"*** amesisitiza Prof. Mbarawa kwa wanahabari.

Aidha, Wizara imejipanga kuhakikisha inawezesha wakandarasi wazawa na wahandisi wanawake kupata kazi na utaalam ili kuwawezesha kushiriki na kuendeleza kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa nchi.

Kuhusu maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) sehemu ya kwanza inayoanzia Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300) Prof. Mbarawa amesema kuwa majaribio ya reli hiyo yanatarajiwa kuanza Mwezi Septemba, 2022.

Akifafanua zaidi kuhusu upanuzi wa Bandari Dar es Salaam amesisitiza kuwa ujenzi wa gati namba 8-11 unaenda sambamba na upanuzi wa gati namba 1-2 katika Bandari ya Tanga ili kuziwezesha bandari hizo kufanya kazi kwa ufanisi.

Kuhusu utunzaji wa miundimbinu ya barabara na madaraja, Waziri Mbarawa amesema Wizara itaendelea kujenga mizani ya kisasa ili kudhibiti magari yanayozidisha uzito ili kuilinda miundominu hiyo.

Zaidi ya Km 1500 za barabara za lami pamoja na madaraja makubwa manne yanaendelea kujengwa katika Bajeti ya Sekta ya Ujenzi, wakati katika Sekta ya Uchukuzi ujenzi wa njia ya reli kipande cha Tabora – Isaka Km.165 na Tabora – Kigoma Km. 411 zinatarajiwa kuanza ujenzi wake.

# Serikali Kuendelea Kuwekeza Tazara

Serikali imesema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga zaidi ya bilioni 12 kwa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo ya ndani na nje ya nchi hususani inayopitia bandari ya Dar es Salaam.

Akizungumza jijini Mbeya mara baada ya kutembelea stesheni, karakana na mgodi wa uzalishaji kokoto wa Kongolo, Naibu Waziri Atupele Mwakibete amesema TAZARA imekuwa ikisafirisha mzigo wa Zambia, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hivyo ili kuongeza idadi ya mzigo Serikali imeendelea kutenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha mzigo unawafikia walaji kwa wakati kupitia miundombinu bora.




*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete (kulia) akitoa maelekezo kwa Naibu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), Mhandisi Christopher Shiganza (wa pili kushoto) na Meneja wa Karakana ya TAZARA-Mbeya Mhandisi Ezekiel Mong'ateko (kushoto) wakati alipotembelea karakana hiyo Mkoani Mbeya.*

> Nchi Jirani zinazotuzunguka zinatumia sana reli hii, na wateja hawa ni muhimu sana kuendelea kuwashawishi kutumia reli hii kupitia miundombinu mizuri na tusisahau biashara ni ushindani hivyo lazima tuliweke hili la maboresho kama kipaumbele

**Atupele Mwakibete**
*Naibu Waziri wa Uchukuzi*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete (kushoto) akimsikiliza Meneja wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), Fuad Abdalla kuhusu maboresho yanayofanyika stesheni za TAZARA, wakati Naibu Waziri alipotembelea Stesheni ya reli hiyo Mkoani Mbeya*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akimsikiliza Msimamizi wa Uchimbaji na Uchongaji wa miamba, Kyando Ndalupia kuhusu uchimbaji unavyofanyika katika mgodi wa kokoto wa Kongolo, wakati Naibu Waziri alipotembelea mgodi huo ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) Mkoani Mbeya.*

Naibu Waziri Mwakibete amesema pamoja na uwekezaji mkubwa unaofanywa amewataka TAZARA kuhakikisha wanafanya ukarabati wa mara kwa mara wa stesheni zao nchini ili kupunguza changamoto mbalimbali zilizopo kwa sasa ikiwemo upungufu wa viti vya kukalia kwa abiria wanaposubiri kuingia kwenye treni.

Aidha, Naibu Waziri Mwakibete amesema ili mgodi wa Kongolo kujiendesha kwa faida ni wakati muafaka kwa TAZARA kuwa na mpango Madhubuti wa biashara ili kutumia vifaa vinavyonunuliwa kwa tija.

Kwa upande Mbunge wa Kyela na Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Mbeya, Ally Jumbe ameipongeza TAZARA kwa kuendeleza juhudi za mara kwa mara za ukarabati kwenye njia na kuhakikisha kuwa treni zinakuwepo na kuondoka kwa wakati.

Naye Meneja wa TAZARA Mkoa wa Tanzania Fuad Abdalla amesema miongoni mwa mikakati ambayo imeendelea kuchukuliwa ili kuongeza ufanisi na kuongeza pato ni pamoja na Mamlaka kuingia makubalino maalum na makampuni binafsi ikiwemo kampuni ya Calabash ili kuhakikisha kuwa reli hiyo inatumika wakati wote.

Meneja Fuad ameongeza kuwa TAZARA pamoja na changamoto za uchache wa vichwa vya treni na behewa Mamlaka imeendelea kuhakikisha inatumia vizuri miundombinu iliyopo kwa kutoa huduma za viwango kwa kusafirisha abiria na mizigo kwa wakati.

Naibu Waziri Wa Uchukuzi Atupele Mwakibete yuko Mkoani Mbeya kwa ziara ya siku tatu kukagua miradi na miudnombinu inayotekelezwa na kusimamiwa na Sekta hiyo.




*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete (kulia) akimsikiliza Meneja wa Karakana ya TAZARA-Mbeya, Mhandisi Ezekiel Mong'ateko kuhusu maendeleo ya ukarabati wa vichwa vya treni wakati Naibu Waziri alipotembelea Karakana hiyo Mkoani Mbeya.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akiangalia moja ya mitambo inayotumika kaboresha vipuri mbalimbali vya vichwa na mabehewa katika karakana ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), Mkoani Mbeya.*



# “Tumieni Uwepo Wa Barabara za Lami Kuwekeza” Eng. Kasekenya

Na **Shukuru Senkondo** - WUU

“

**Zitunzeni barabara hizi za lami kwa kuhakikisha mnazitumia kuchochea maendeleo na kukuza uchumi wenu**

**Eng. Godfrey Kasekenya**
*Naibu Waziri wa Ujenzi*

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya amezungumzia umuhimu wa watanzania kutumia fursa zinazotokana na ujenzi wa miundombinu hususan barabara za lami kuwekeza katika nyanja za kilimo, mifugo, uvuvi, na utalii ili kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.

Akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara katika mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Mara Naibu Waziri Kasekenya amesema Serikali inatumia fedha nyingi katika ujenzi wa barabara za lami hivyo ni wajibu wa wananchi kunufaika kijamii na kiuchumi kutokana na uwekezaji unaofanywa na Serikali katika barabara hizo.

Amebainisha kuwa Serikali itaendelea kujenga barabara za lami kimkakati ili kuwapunguzia wananchi gharama za kusafiri umbali mrefu kwa kujenga njia mbadala na fupi akitolea mfano wa barabara ya Mwigumbi-Maswa-Bariadi ambayo ujenzi wake katika sehemu zinazofanyiwa maboresho utakamilika Septemba mwaka huu.

Kuhusu barabara ya Nyamuswa-Bulamba KM 56,4 ambayo ni sehemu ya barabara ya Nyamuswa-Bunda-Kisorya-Nansio KM 121.9 mkoani Mara Naibu Waziri Kasekenya ameelezea kuridhishwa na kasi ya ujenzi wake na kumtaka mkandarasi anayejenga barabara hiyo China Civil Engineering Construction Cooperation (CCECC), kuongeza kasi ya ujenzi na kuhakikisha anajenga vivuko katika maeneo ya makazi na yenye huduma za jamii ili kulinda kingo za barabara hiyo.

Amebainisha kuwa nia ya Serikali ni kuunganisha barabara za mkoa wa Mara na Arusha ili kukuza utalii wa kisasa kufuatia ongezeko kubwa la watalii katika hifadhi za Serengeti na Ngorongoro.

Naye Mbunge wa Bunda Mhe. Boniface Getere ameipongeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa namna inavyofuatilia miradi ya ujenzi wa barabara mkoani Mara na kumhakikishia Naibu Waziri elimu ya kuilinda na kuitumia miundombinu hiyo itatolewa ili kuiwezesha kudumu kwa muda mrefu.




*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akifafanua jambo kwa wakazi wa mji wa Mugumu wilayani Serengeti alipokagua barabara ya Mogabiri-Nyamongo-Tarime inayotarajiwa kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami hivi karibuni*



*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akisisitiza jambo kwa Mhandisi Paul Margwe wa Wakala wa Barabara Tanzania TANROADS mkoa wa Mara wakati wa ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Nyamuswa-Bulamba KM 56.4.*



*Muonekano wa barabara ya Nyamuswa-Bulamba KM 56.4 mkoani Mara ambayo ujenzi wake kwa kiwango cha lami unaendelea.*



# Barabara ya Saadani Hadi Tanga Kuchochea Usafirishaji

Na **Deniza Cyprian** - WUU

Imeelezwa kuwa kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Tungamaa – Mkwaja – Mkange (km 95.2), ikiwemo na kilometa 3.7 za mchepuo wa barabara ya Kipumbwi inayojengwa kwa kiwango cha lami itafungua fursa za usafiri na usafirishaji katika mwambao wa Tanga na mikoa ya jirani.

Hayo yamesemwa mkoani Tanga na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alipoutembelea na kuukagua mradi huo unaogharimu takribani shilingi Bilioni 94.53 ambao umeanza mwezi Aprili, 2022.

"Mradi huu ni mradi wa pamoja kati ya nchi yetu na nchi ya Kenya ambayo itamruhusu msafirishaji kutoka kuanzia Bagamoyo – Saadani – Tanga – Horohoro/Lungalunga nchini Kenya – Mombasa mpaka Lamu kupitia barabara hii ambapo na wenzetu wanaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa sehemu yao", amefafanua Prof. Mbarawa.

Ameongeza kuwa barabara hiyo itafungua fursa nyingi iwemo Sekta ya Utalii kwani itawezesha watalii kutoka nchi za jirani na kuja kutembelea hifadhi ya Saadani na visiwa vya Zanzibar kwaurahisi.

Aidha, amemtaka mkandarasi kujipanga vyema katika mpango kazi wake ili kukamilisha mradi huo ambao unasubiriwa kwa hamu kubwa na wananchi wa mikoa ya Pwani na Tanga kwaajili ya kuimarisha shughuli za kiuchumi.

Kuhusu fidia za wananchi waliopisha mradi huo, Waziri Mbarawa ameutaka Wakala wa Barabara (TANROADS), kuhakikisha wanatoa elimu kwa baadhi ya wananchi ambao wanakuwa na ukakasi wa kupisha maeneo ya miradi inayoendelea kutekelezwa hapa nchini na hivyo kupelekea miradi ya miundombinu kutokukamilika kwa wakati.

"Nichukue fursa hii kwa watanzania wenzangu waliopitiwa na mradi huu waruhusu ujenziu endelee na mkandarasi afanye kazi yake kama wana malalamiko waje Wizarani kwa utaratibu na watasikilizwa", amesisitiza Prof. Mbarawa.

Kwa upande wake, Meneja wa TANROADS mkoa wa Tanga, Eng. Eliazary Rweikiza ameeleza kuwa hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 6.23 ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa kambi

ya mkandarasi umekamilika kwa asilimia 100 na kambi ya MhandisiMshauriimefikiaasilimia 75.

Eng. Rweikiza ameongeza kuwa kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na kusafisha barabara, uchimbaji wa udongo, kuweka tabaka la kifusi na kuendelea kutengeneza makalvati ya zege katika barabara hiyo.

Ujenzi wa barabara ya Tungamaa – Mkwaja – Mkange (km 95.2), ikiwemo na kilometa 3.7 za mchepuo wa barabara ya Kipumbwi kwa kiwango cha lami unatekelezwa na muda wa miezi 36 na mkandarasi China Railway 15 Burea Group Corporation na kusimamiwa na Mhandisi Mshauri kutoka Kampuni ya Beza Consulting Engineering kwa kushirikiana na Chiel Engineering naAfrisa Consulting wa Ethiopia.



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akisisitiza jambo kwa mkandarasi wa Kampuni ya China Railway 15 Bureau Group Corporation (hayupo pichani), wakati akikagua mradi wa ujenzi wa barabara ya Tungamaa – Mkwaja – Mkange (km 95.2), ikiwemo na kilometa 3.7 za mchepuo wa barabara ya Kipumbwi kwa kiwango cha lami, mkoani Tanga.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour (wa nne kutoka kulia), akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Njombe.*



# Kamati Yaitaka Serikali Kuiwezesha NIT

Na **Mwandishi Wetu** - WUU

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Selemani Kakoso ameelezea umuhimu wa Serikali kukiwezesha kikamilifu Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ili kiwe cha Kimataifa.

Akizungumza mara baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji ya Chuo hicho iliyowasilishwa katika kamati yake Mhe. Kakoso amesema NIT ni miongoni mwa vyuo vinavyofanya vizuri nchini hivyo kiwezeshwe kuwa na wataalam, watumishi na vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunziaa ili kiweze kufikia malengo na kuimarisha sekta ya uchukuzi hapa nchini.

“Hakikisheni idadi ya watumishi inaongezwa ili wanafunzi wengi wa ndani na nje ya nchi wajiunge na Chuo hiki muhimu na hivyo kuliwezesha taifa kupata wataalam wa kutosha watakaosimamia nyanja zote za usafirishaji na uchukuzi nchini,” amesema Mwenyekiti Kakoso.

Aidha ameitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kukitangaza Chuo hicho na kukiwezesha kutoa kipaumbele katika kufundisha mafundi stadi na sanifu ili kuziba pengo lililopo kati na mafunzi stadi, sanifu na wahandisi nchini.

Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete amesema Serikali ina mikakati ya dhati kuiwezesha NIT kuwa Chuo cha mfano kwa kuhakikisha kinatoa kozi zote zinazohusu usafiri wa ardhini, maji na anga na hivyo kuwawezesha wataalam watakaohudumu kwenye uwekezaji wa miradi ya reli, meli, ndege na magari kupata stadi zao hapa nchini.

Katika hatua nyingine Kamati hiyo ya Bunge imeitaka Sekta ya Uchukuzi kuhakikisha inasimamia kikamilifu Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kwenye eneo la mapato, tehama na masoko ili kuiwezesha bandari kufanya kazi kwa ufanisi na kuongeza mapato.

“Kukamilika kwa miradi ya upanuzi wa bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na kwenye Maziwa ya Tanganyika, Nyasa kutaongeza ufanisi wa bandari nchini’ amesisitiza Mwenyekiti Kakoso.



**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imepitia taarifa ya utendaji kazi ya taasisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), na kuhimiza ushirikiano miongoni mwa watumishi wa taasisi ili kufikia malengo.**





# TANROADS Waaswa Kuwa Wabunifu Kupunguza Gharama za Ujenzi

Na **Mwandishi Wetu -** WUU

Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), wameaswa kuwa wabunifu na mstari wa mbele katika ulindaji wa miundombinu inayojengwa kwa gharama kubwa na Serikali pamoja na kutumia malighafi zinazopatina sehemu husika ili kupunguza gharama zinazotumika katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, madaraja na mizani hapa nchini.

Agizo hilo limetolewa mkoani Njombe na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour, katika kikao kazi na watumishi wa Wakala huo ambapo amesisitiza weledi, ubunifu, matumizi ya kisasa ya TEHAMA ili kuleta ufanisi katika utendaji wao kazi.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour, akizungumza na watumishi wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Njombe (hawapo pichani), wakati walipofanya kikao kazi na watumishi hao kuhusu uboreshaji wa utendaji kazi.*

“Nahitaji mabadiliko kwa watumishi wa TANROADS katika matumizi ya teknolojia maana huko kuna vitu vingi vya kujifunza badala ya kupoteza muda kuangalia masuala yasiyokuwa na tija katika utendaji kazi wenu”, amesisitiza Balozi Aisha.

Ameongeza kuwa Wizara imepanga kutoa motisha kwa watumishi ambao watakuja na mawazo mapya yenye kuleta tija katika uboreshaji na usimamizi wa miundombinu iliyopo na inayoendelea kutekelezwa hapa nchini.

“Hakikisheni mnaibua vipaji vya watumishi wenu mahala pa kazi kwa kuhakikisha kila mtumishi aliyeajiriwa anatekeleza majukumu yake ipasavyo na kuondoa dhana ya watu wachache kuonekana bora zaidi”, amesema Katibu Mkuu huyo.

Awali akitoa taarifa ya mkoa huo, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Njombe Mhandisi Kipembawe Msekwa ameeleza kuwa ujenzi wa barabara ya Njombe – Makete na Itoni – Ludewa – Manda zinazounganisha Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya (Ludewa na Makete) tayari zimeanza kutoa matunda katika shughuli za usafiri na usafirishaji wa abiria na mazao kutoka shambani na kukuza uchumi wa mkoa.

“Barabara hizi zimepelekea muda wa safari kupungua hadi wastani wa saa mbili (kutoka Makete) na saa tatu (kutoka Ludewa) ambapo hapo awali hasa kipindi cha masika muda wa safari ulikuwa ni mwendo wa siku nzima”, amefafanua Mhandisi Msekwa.

Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Njombe unahudumia matengenezo ya barabara yenye jumla ya (km 1,188.23) kati ya hizo (km 403.420) ni Barabara Kuu na (km 784.810) ni Barabara za Mkoa.

# TPA Watakiwa Kuzingatia Mazingira Bandari Mtwara

Na **Christopher Philemon -** WUU



*Katibu Mkuu- Uchukuzi Gabriel Migire (kushoto) akitoa maelekezo kwa Kaimu Meneja wa Bandari ya Mtwara James Ng'wandu mara baada ya kutembelea Bandari ya Mtwara.*

Katibu Mkuu (Sekta ya Uchukuzi) Gabriel Migire ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kushirikiana na taasisi zote zinazohusika kushirikiana na kuhakikisha Usalama wa Mazingira unazingatiwa kwenye ushushaji, utunzaji na upakiaji wa Makaa ya Mawe unazingatiwa.

Katibu Mkuu Migire amesema hayo mara ya kukagua eneo linalotunzwa Makaa ya Mawe katika Bandari ya Mtwara na kubaini changamoto ya vumbi jingi katika utunzaji wa Makaa hayo kabla ya kusafirishwa nje ya nchi kupitia bandari hiyo.

"Kuna mzigo mkubwa sana wa makaa ya mawe hapa lakini bado hatujaweza kudhibiti vumbi la mkaa haya lisitoke nje ya bandari, hivyo TPA shirikianeni na wadau wote muhimu ili kuweka mazingira mazuri kwa mzigo usije kuwa na changamoto zaidi za kimazingira na tukaleta athari kwa wanauhudumia mzigo huu na wananchi nje ya bandari hii' amesisitiza Katibu Mkuu Migire.

Katibu Mkuu Migire zoezi hilo lisiishie kwenye Makaa ya Mawe litazamwe na kwenye utunzaji wa bidhaa zote ambazo kwa sasa zinasafirishwa kwa wingi kupitia bandari hiyo zitazamwe upya ikiwemo Korosho na Simenti ili kutokusanya mapato na kuacha changamoto nyingine bila kushughulikiwa.

Kwa upande wake Msimamizi wa Usafirishaji wa Makaa ya Mawe kutoka kampuni ya Makaa ya Mawe ya Ruvuma, Abdallah Dadafi amesema kuwa tayari wamechukua hatua mbalimbali za kunusuru athari hizo ikiwemo kununua magari maalum yatakayotumika kupunguza ya vumbi linalotokana na ushushaji, utunzaji na upakiaji wa makaa hayo.

Naye Meneja wa Bandari Mtwara James Ng'wandu amesema kuwa kwa mamlaka hiyo imejiwekea lengo la kusafisha tani elfu sitini ya Makaa ya mawe ambapo mpaka sasa imefanikiwa kusafirisha tani elfu arobaini kwa mwezi ambazo husafirishwa kwa wingi kuelekea nchini Nigeria na Bara la Asia.

Katibu Mkuu Myuko mkoani Mtwara kutembelea na kukagua miradi ya taasisi zilizo chini ya Sekta hiyo.



*Katibu Mkuu-Uchukuzi Gabriel Migire (kulia) akizungumza na wafanyakazi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara wakati alipotembelea Kiwanja hicho Mkoani Mtwara.*



*Gari maalum likimwaga maji kwenye Makaa ya Mawe yaliyohifadhiwa katika Bandari ya Mtwara ili kupunguza vumbi. Zaidi ya Tani elfu ishirini za makaa hayo kusafirishwa kila mwezi kupitia bandari ya Mtwara kuelekea nchi za Nigeria na Bara la Asia.*

# Meli za TPA Mwarobaini wa Usafirishaji wa Abiria na Mizigo Ziwa Nyasa



Na **Biseko Ibrahim -** WUU

Imeelezwa kuwa kukamilika kwa ukarabati na kuanza kufanya kazi kwa meli ya MV. Mbeya II kutarahisisha shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa wasafirishaji walioko katika Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Njombe na Nchi Jirani ya Malawi.

Akizungumza Wilayani Kyela Naibu Waziri wa Uchukuzi Atupele Mwakibete amesema wananchi wa Mikoa hiyo wamekuwa wakilazimika kutumia mabasi bila na kuwa na njia mbadala ya usafiri hususani kwa wale wanaoishi mikoa hiyo hivyo kukamilika na kuanza kazi kwa meli hiyo kutawapa ahueni ya usafiri.

"Niwapongeze Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kwa kuhakikisha meli hizi zinakarabatiwa na kuanza kutoa huduma baada ya kupata changamoto na kusimama kwa zaidi ya miezi 5, kurejea kwa meli hizi sasa watakuwa na uwezo wa kusafiri kwa wakati na kwa gharama nafuu kwa kutumia meli hii' amesema Naibu Waziri Mwakibete



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete na Mbunge wa Kyela Ally Jumbe wakishuka katika meli ya MV Mbeya II mara baada ya kukagua meli hiyo, Wilayani Kyela Mkoani Mbeya.*

Naibu Waziri Mwakibete amewataka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) na Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kuhakikisha wanashirikiana kwa karibu ili kushughulikia changamoto zote zitakazojitokeza kabl aya makabidhiano kati ya TPA na MSCL.

Aidha, Naibu Waziri Mwakibete amewataka TPA kutafuta masoko ili kupata mzigo mkubwa kwa wafanyabiashara ikiwemo Simenti na Makaa ya Mawe ili meli hizo ziweze kuwa na tija na kuongeza pato la Mamlaka.

Kwa upande wake Katibu wa CCM Wilaya ya Kyela Gervas Ndaki ameishukuru Serikali kwa kuhakikisha meli hizo zinarejea kutoa kutoka huduma katika mikoa iliyo katika Ukanda wa Ziwa Nyasa na kuahidi kuhamasisha wananchi kutumia meli hizo kufanya safari zao.



Naibu Waziri wa Uchukuzi Atupele Mwakibete (wa pili kustoto) akitoa maelekezo kwa Watendaji wa Taasisi za Sekta ya Uchukuzi, wakati alipokagua meli za MV. Mbeya II Wilayani Kyela Mkoani Mbeya.

Naye Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa Manga Gasaya amesema tangu kuanza kutoa huduma kwa meli hiyo idadi ya abiria imekuwa ikiongezeka siku hadi siku na kumuhakikisha Naibu Waziri Mwakibete kuwa TPA ndani ya wiki mbili itatuma wawakilishi kwenda kuzungumza na wafanyabiashara wa nchini Malawi.

Meneja Gasaya ameongeza kuwa TPA kwa sasa meli hizo zinaendeshwa na Mamlaka hiyo na kumuahidi Naibu Waziri Mwakibete kuwa TPA iko kwenye hatua za mwisho za kukabidhi meli hizo kwa MSCL kwa ajili ya uendeshaji wake kama Serikali ilivyoelekeza.

Serikali kupitia TPA kwa mkoa wa Mbeya imejengwa meli tatu ikiwemo MV. Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200, MV Ruvuma yenye uwezo wa kubeba tani 1000 na MV Ruvuma yenye uwezo wa kubeba tani 1000 meli ambazo zinasafirisha abiria na mizigo kwa Mikoa inayozunguka Ziwa Nyasa na Nchi Jirani ya Malawi.



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akisalimiana na Viongozi wa Wilaya ya Kyela na Watendaji wa Taasisi za Sekta ya Uchukuzi, alipowasili Wilayani Kyela kwa ziara ya siku moja Mkoani Mbeya.*



# Wahandisi na Wakandarasi Wazawa Watakiwa Kuchangamkia Fursa

Na **Mwandishi Wetu** - WUU

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema Serikali itaendelea kuwasajili na kuwawezesha wakandarasi na wahandisi wazawa ili waweze kunufaika na fursa za miradi ya ujenzi inayoendelea nchini.

Amesema hayo jijini Dodoma, katika taarifa yake kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na kusisitiza kuwa nia ya Serikali ni kuhakikisha wahandisi na wakandarasi wazawa wanaungana katika vikundi ili wanufaike na fursa za kujengewa uwezo wa utaalamu, mitaji, mitambo na uzoefu ili waweze kupata kazi nyingi na kukuza uchumi wao na wa Taifa kwa ujumla.



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Mha. Godfrey Kasekenya, akisisitiza jambo wakati alipokutana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu jijini Dodoma.*



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akisisitiza jambo wakati alipokutana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu jijini Dodoma.

> "Tumejipanga kuhakikisha wahandisi na wakandarasi wetu wanabobea katika usimamizi wa miradi na mikataba ili kuwawezesha kupata miradi mingi na kujenga hazina ya wataalam wa Sekta ya Ujenzi hapa nchini

**Prof. Makame Mbarawa**
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*

Amesema Serikali inajipanga kujenga barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro ili kupunguza msongamano wa magari yanayoingia na kutoka jijini Dar es Salaam na kuhakikisha barabara zote kuu na za mikoa zinakuwa katika kiwango bora na kupitika kipindi chote cha mwaka.

Akizungumza katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Selemani Kakoso, amehimiza Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB), kusimamia vizuri wahandisi wanaosimamia miradi ya Serikali kujengwa katika viwango bora na hivyo kulinda fedha za Serikali kwa kuiwezesha kudumu kwa muda mrefu.

Aidha, amezungumzia umuhimu wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) kuwezeshwa kupata fedha za kutosha ili barabara zinazojengwa kwa fedha nyingi ziweze kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na hivyo kuondoa usumbufu kwa wananchi na kuvutia wadau wengi kutumia barabara za hapa nchini.



Katibu Mkuu wa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Balozi Mha. Aisha Amour, akifafanua jambo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara wakati wa kuwasilisha taarifa kwa kamati hiyo jijini Dodoma.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo anayesimamia Sekta ya Ujenzi, Balozi Mha. Aisha Amour, ameihakikishia Kamati hiyo kuwa Wizara imejipanga kupambana na rushwa na uzembe katika mizani zote nchini na itaendelea kutoa elimu kwa maofisa wanaosimamia mizani, wasafirishaji na watumiaji wa barabara wakati wote.

Amesema katika kutengeneza uwiano wa wahandisi na wakandarasi, Wizara inaendelea na juhudi ya kuhakikisha wahandisi na wakandarasi wanawake wanasajiliwa kupata fursa za elimu na kushiriki katika miradi ya ujenzi kwa nyanja zote.



*Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakimsikiliza Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Suleiman Kakoso, wakati wa uwasilishaji wa taarifa za Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, jijini Dodoma.*

# Kiwanja cha Ndege Kigoma Kupanuliwa Kufikia Mita 3000

Na **Biseko Ibrahim -** WUU




*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete (kushoto) akimsikiliza Kaimu Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, Mbura Daniel kuhusu utendaji wa Kiwanja hicho wakati Naibu Waziri huyo alipotembelea Kiwanja cha Ndege hicho Mkoani Kigoma.*

Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kwa kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kutoka ya sasa yenye mita 1800 hadi kufikia mita 3000 kutaruhusu kiwanja hicho kuhudumia ndege kubwa zaidi zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 150.

Akizungumza mkoani Kigoma mara baada ya kutembelea Kiwanja hicho Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete amesema Serikali imedhamiria kufufua usafiri wa anga nchini kwa kununua ndege na kuboresha viwanja vya ndege ili kurahisisha shughuli za biashara na utalii baina na mikoa na nchi Jirani.

“Serikali inaendelea na mkakati wake wa kuendelea kujenga viwanja vya ndege nchini hasa ukizingatia Mhe Rais alifanya filamu ambayo matokeo yake yameanza kuonekana na hatuna budi kuendelea kujenga miundombinu rafiki na mizuri kwenye kila eneo’ amesema Naibu Waziri Mwakibete.



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akitoa maelekezo kwa Watendaji wa taasisi za Sekta ya Uchukuzi wakati alipotembelea Kiwanja cha Ndege hicho Mkoani Kigoma.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akitoa maelekezo kwa Meneja wa Shirika la Ndege la Ndege Tanzania (ATCL) Mkoa wa Kigoma Mwantumu Kipwasa, wakati alipotembelea Kiwanja cha Ndege cha Kigoma.*

**Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege unatarajiwa kugharimu zaidi ya bilioni 50 na fedha hizo zitahusisha upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho, uzio na malipo ya fidia.**

Naibu Waziri Mwakibete amewapongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa kuendelea kufanya maboresho katika viwanja mbalimbali nchini na kuwataka kuendelea kushirikiana na vyombo vingine ili kuhakikisha wanadhibiti usafirishaji wa nyara za Serikali.

Kwa upande wake Mbunge wa Kigoma Mjini Kilumbe N'genda ameishukuru Serikali na kusema Kigoma itaendelea kufunguka kibiashara na kukuza pato kwani nchi Jirani kama Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Burundi zinafanya sana biashara na mkoa wa Kigoma.

Kaimu Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma Mbura Daniel amesema idadi ya miruko ya ndege imekuwa ikiongezeka kwani hicho pamoja na kutumiwa na ndege za ratiba kama Air Tanzania pia mashirika mbalimbali hukitumia kiwanja hicho kwa kuja kufanya biashara na mikutano ya Kimataifa.

Meneja wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Mkoa wa Kigoma Mwantum Kipwasa amesema shirika linasubiri kwa hamu kukamilika kwa upanuzi huo ili kuleta ndege kubwa kwani idadi ya abiria imelazimisha shirika hilo kuwa na ndege kila siku ili kukidhi haja ya wateja wao.

# Septemba Mwaka Huu Magari Kupita Daraja Jipya la Wami

Na **Segolena Francis** - WUU



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema kuwa Serikali inatarajia kuanza kuruhusu magari kupita juu ya daraja jipya la wami, lililopo mkoani Pwani ifikapo mwezi Septemba mwaka huu.

Hayo yamesemwa na Waziri huyo wakati akikagua hatua za maendeleo ya daraja hilo ambapo pamoja na mambo mengine amemtaka mkandarasi kukamilisha kazi ndogo ndogo zilizobakia katika daraja hilo ili kurahisisha matumizi salama ya watumiaji wa daraja hilo.

"Hadi sasa kazi zinaendelea vizuri, ni matumaini yangu hadi kufikia tarehe 20 Septemba, mtakuwa mmeshakamilisha kazi zilizobaki ili mimi niweze kuruhusu magari kupita", amesema Waziri Prof. Mbarawa.

Ameeleza kuwa mradi huo ambao umefikia asilimia 86 katika utekelezaji wake unajumuisha ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 513.5 pamoja na ujenzi wa barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 3.8.

Aidha, amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha za miradi ya kimkakati na kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji nchini.

Akitoa taarifa ya mradi, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Pwani Eng. Heririsper Mollel, ameeleza kuwa kwa upande wa ujenzi wa daraja mkandarasi amekamilisha ujenzi wa sehemu ya chini ya daraja kwa asilimia 100 na sehemu ya juu amekamilisha tabaka la juu la lami mita 256 kati ya mita 513.5 ambayo ni sawa na asilimia 50 ya urefu wa daraja.

Ameongeza kuwa kazi nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa makalvati makubwa matatu na madogo saba na uwekaji wa mabomba 188 ya maji kati ya 206 ambayo ni sawa na asilimia 91.

Kuhusu ujenzi wa barabara unganishi Eng. Heririsper amesema kuwa hadi sasa kilometa 3.4 za ujenzi wa tabaka la lami la chini zimekamilika.

**Ujenzi wa Daraja jipya la Wami unagharimu zaidi ya shilingi Bilioni 75 ambazo ni fedha za Serikali kwa asilimia 100 na unatekelezwa na mkandarasi Power Construction Corporation kwa muda wa miezi 48.**




# Naibu Waziri Mwakibete Atoa Mwezi Ukaguzi Mt. Sangara

Na **Mwandishi Wetu** - WUU

Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete ametoa mwezi mmoja kwa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kutumia wataalam alionao kufanya tathmini ya kina kwa vifaa vyote vilivyofungwa kwenye Meli ya MT. Sangara na kuchukua hatua kwa taarifa itakayowasilishwa.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya ukarabati huo mjini Kigoma na kubaini uwepo wa changamoto ya baadhi ya vifaa kuwa Naibu Waziri Mwakibete amesema Serikali haitaipokea meli hiyo itakapokabidhiwa na kugundulika kuwa na mapungufu.

"Nawahakikishia vifaa vyote vilivyofungwa humu endapo itabainika baadae kuwa ni chakavu au vimeshatumika, Serikali itachukua hatua stahiki kwa wote waliohusika sababu changamoto zote za vifaa zinatakiwa kurekebishwa sasa hivi" amesisitiza Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete amesisitiza umuhimu wa watalam kukagua kwa karibu ukarabati huo mkubwa unaofanyika ili kuhakikisha maboresho yote yanayofanyika yanafanywa kwa kufuata vipengele vya mkataba.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kigoma Ester Mahawe ameishukuru Serikali kwa kufanya ukarabati wa meli hiyo na kusema kukamilika kwake kutarahisisha shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa mikoa inayozungukwa na Ziwa Tanganyika na nchi Jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia.

Kwa upande wake Kaimu Mtendaji Mkuu wa MSCL Philip Bangabilana amesema MSCL itaendelea kumsimamia kwa karibu Mkandarasi na kuhakikisha mapungufu yote yanarekebishwa kwa wakati kulingana na mkataba unavyoeleza.

Bangabilana ameongeza kuwa kwa sasa mradi wa Ukarabati wa MT. Sangara umefikia asilimia 66 na unatarajiwa kukamilika mapema mwezi Novemba mwaka huu na kwa mwaka 2022/23 Serikali imetengea fedha kwa ajili ya meli nyingine mpya mbili.



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete (wa pili kushoto) akitoa maelekezo kwa Uongozi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), wakati alipokagua maendeleo ya ukarabati wa meli ya MT. Sangara unaofanywa katika bandari ya Kigoma. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya MSCL Meja Jenerali Julius Mbungo.*



# Ujenzi BRT II Wafikia Asilimia 66.6



Na **Mwandishi Wetu** - WUU

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema ujenzi wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II), Awamu ya Pili kutoka Mbagala hadi Gerezani umefikia asilimia 66.6 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2023.

Prof. Mbarawa amesema hayo jijini Dar es Salaam mara baada ya kukagua ujenzi wa mradi huo ambapo amefafanua kuwa kazi zinaenda vizuri huku ikitarajiwa kuwa mradi huo kukamilika kwa muda uliopangwa ili uweze kupunguza msongamano wa magari na kurahisisha usafiri.

"Nimefurahi kazi inaenda vizuri ila bado nitakuwa nikija hapa kukagua mradi huu mara kwa mara ili kuhakikisha mkandarasi anamaliza kwa wakati na viwango kwa sababu mradi huu ni muhimu sana katika kurahisisha usafiri na kupunguza msongamano", amesisitiza Prof. Mbarawa.

Aidha, Prof. Mbarawa amemtaka mkandarasi wa mradi huo kuhakikisha anakamilisha upande wa pili wa barabara za juu (flyover) ya Chang'ombe na Kurasini ifikapo mwezi Oktoba ili kuruhusu magari kupita juu huku kazi nyingine zilizobakia zikiendelea.

Amemtaka pia kukamilisha ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 80 eneo la BP ifikapo mwezi Desemba 2022 na madaraja mengine kukamilishwa mwezi Januari, 2023 ili kupunguza changamoto ya msongamano wa magari katika maeneo hayo.

Pamoja na hayo amewataka wananchi waliopo karibu na mradi huo kutoa ushirikiano kwa mkandarasi ili mradi huo umalizike mapema iwezekanavyo.

Kwa upande wake, Msimamizi wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II), Eng. Frank Mbilinyi, amesema kuwa wanatarajia Daraja lililopo Bandarini kumalizika na magari kuanza kupita mwezi Oktoba mwishoni wakati madaraja mengine yameshakamilika kwa upande mmoja na magari yameruhusiwa kupita.



*Msimamizi wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II), Eng. Frank Mbilinyi, akitoa maelezo kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, wakati Waziri huyo alipokagua maendeleo ya mradi huo, jijini Dar es Salaam.*



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akikagua hatua za ujenzi wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II), Awamu ya Pili unaoanzia eneo la Mbagala hadi Gerezani ambao umefikia asilimia 66.6 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2023.

**Mradi huu ni moja ya mkakati ya Serikali ya kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam ambapo unahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 20.3, Daraja kubwa la Waenda kwa miguu eneo la Mbagala, vituo vya mabasi 27, karakana ya mabasi 1, vituo vikuu viwili vya mabasi (Terminals) eneo la Kariakoo na Mbagala, vituo vya mlisho (feeder station) 5 pamoja na barabara za juu (flyover) 2 eneo la Chang'ombe na Uhasibu ambazo zitagharimu takribani Shilingi Bilioni 217.**



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akitoa maelekezo kwa mkandarasi wa kampuni ya Sino Hydro Cooperation anayetekeleza mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II), Awamu ya Pili unaoanzia eneo la Mbagala hadi Gerezani mara baada ya kufika na kukagua maendeleo yake, jijini humo. Mradi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2023.



# Abiria Kiwanja cha Ndege Songwe Waongezeka

Na **Mwandishi Wetu** - WUU

**Abiria wanaotumia Kiwanja cha Ndege cha Songwe wameripotiwa kuongezeka kutoka abiria elfu sitini na tisa (69,000) kwa mwaka 2020/2021 hadi elfu themanini na tano (85,000) kwa mwaka 2021/22 ikiwa ni matokeo ya upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe.**

Akizungumza jijni Mbeya mara baada ya kukagua upanuzi wa Kiwanja hicho pamoja na Wabunge wa Mkoa huo Naibu Waziri wa Uchukuzi Atupele Mwakibete amesema kukamilika kwa mradi huo kumefanya kiwanja hicho kufanya kazi kwa saa 24 na hivyo kurahisisha zaidi shughuli za usafirishaji baina ya mkoa huo na mikoa mingine nchini.

"Tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu kwa kuwekeza fedha nyingi kwenye upanuzi wa kiwanja hiki ambapo baadhi ya maeneo ujenzi umekamilika na maeneo mengine kazi zinaendelea kwa kasi", amesema Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete amesema nia ya Serikali ni kuongeza miudombinu rafiki na wezeshi kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo mbalimbali ikiwemo bidhaa za mbogamboga na matunda zinazozalishwa katika mikoa ya nyanda za juu kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi.

Naye Mbunge wa Mbeya Vijijini ambaye pia ni Mwenyekiti wa Wabunge wa Mbeya, Oran Njeza amesema kuwa kiwanja hicho kuwa na miudombinu ya kisasa na uwezo wa kufanya kazi saa ishirini na nne ni fursa kwa wananchi wa mkoa wa Mbeya na mikoa jirani kuongeza kipato kwani biashara zitafanyika wakati wote.

Naye Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Mhandisi Danstan Komba, amesema kwa sasa mradi wa kuongeza urefu wa barabara ya kuruka na kutua, taa na uzio umekamilika kwa asilimia mia moja na ujenzi wa jengo la abiria unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

Mradi wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Songwe umehusisha kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kutoka mita 3000 hadi mita 3330, taa, uzio na jengo la abiria litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 500 kwa wakati mmoja.



*Fundi wa Kampuni ya China Geo-Engineering Corporation akiendelea na ujenzi katika jengo la abiria la kiwanja cha Ndege cha Songwe, jijini Mbeya. Jengo hilo litakapokamilika litaweza kuhudumia abiria 500 kwa wakati mmoja.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi Atupele Mwakibete akizungumza na Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Mhandisi Danstan Komba (katikati) na Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Nikolus Kalenzo, wakati Naibu Waziri huyo alipokagua maendeleo ya Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe jijini Mbeya.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi Atupele Mwakibete (wa tatu kulia), akisisitiza jambo kwa Sehemu ya Wabunge wa Mkoa wa Mbeya wakati walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe jijini Mbeya. Wa pili kushoto ni Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Mhandisi Danstan Komba.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi Atupele Mwakibete (wa tatu kulia) na sehemu ya wabunge wa Mbeya wakimsikiliza Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Mhandisi Danstan Komba kuhusu maendeleo ya mradi wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe, wakati Naibu Waziri huyo alipowaongoza wabunge hao kukagua mradi huo Jijini Mbeya.*



# "Onesheni Uwezo Tuwape Miradi Mingi ya Ujenzi" Eng. Kasekenya

Na **Mwandishi Wetu** - WUU



Imeelezwa kuwa juhudi za Serikali za kuwawezesha kiutaalam, kiuzoefu na kimitaji kwa kuwapa miradi mingi ya ujenzi wakandarasi wa ndani ya nchi zitafanikiwa endapo wakandarasi hao watatambua dhima yao kwa nchi na kufanyakazi kwa bidii na viwango vya juu.

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya ameeleza hayo alipokagua ujenzi wa barabara ya Musoma – Makojo - Busekela yenye urefu wa KM 92 ambayo ujenzi wake kwa kiwango cha lami umeanza sehemu ya Nyambui- Suguti.

"Serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha wakandarasi wa ndani wanakuwa na uwezo na hivyo kujenga miradi mingi na mikubwa ili kukuza uchumi wa nchi na kuongeza fursa za ajira hivyo jitahidini kuongeza bidii na ubunifu", amesema Eng. Kasekenya.
Amemtaka mkandarasi Gemen Engineering Co. Ltd, anayejenga barabara hiyo Km 5 za awali kutoka Nyambui - Suguti, kuhakikisha barabara hiyo inakamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu.

Akizungumzia umuhimu wa barabara hiyo Mkuu wa wilaya ya Musoma Dakta, Khalfan Haule amesema barabara hiyo inayopita eneo la Musoma vijijini ikikamilika litachochea ukuaji wa uchumi kwa wananchi wa mkoa wa Mara kwa kuwa itaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na shughuli za uvuvi.

Amesisitiza kuwa itachochea utalii kwa kuwa inapita pembezoni mwa ziwa Victoria hivyo kuongeza vivutio vya utalii mkoani Mara.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Kasekenya amemtaka Mtendaji mkuu wa Wakala wa Barabara nchini TANROADS Eng. Rogatus Mativila kufanya tathmini na kuja na majibu ya haraka ya namana bora itakayowezesha kasi katika ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Musoma.

Ameelezea kutoridhishwa kwake na kasi ndogo katika ujenzi wa uwanja huo na kusisitiza Serikali haitasita kuchukua hatua kali kwa wote wanaochelewesha miradi ya ujenzi kukamilika kwa wakati.




*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya (wa kushoto), akimsikiliza Eng, Andrew Nyantori kutoka kampuni ya Gemen Engineering Co. Ltd, anayejenga barabara ya Nyambui – Suguti Km 5 kwa kiwango cha lami ambayo ni sehemu ya barabara ya Musoma-Makojo-Busekela Km 92 mkoani Mara, kulia ni Mkuu wa wilaya ya Musoma Dakta, Khalfan Haule.*



*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akitoa maelekezo kwa wataalam wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) na wasimamizi wa ujenzi wa mizani ya Rubana inayojengwa wilayani Bunda.*

# Behewa Mpya Zaidi ya 20 Kuwasili Nchini Septemba



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akitoa maelekezo kwa Uongozi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), wakati alipotembelea stesheni ya Reli ya Kigoma.*

Na **Mwandishi Wetu** - WUU

Serikali imesema mabehewa mapya ya abiria zaidi ya 20 ya reli ya kati yanatarajiwa kuwasili mapema mwezi Septemba mwaka huu kutokea Nchini Korea Kusini lengo likiwa kupunguza changamoto ya upungufu uliopo wa mabehewa hususani kwa njia ya Mpanda na Kigoma.

Akizungumza Mkoani Kigoma Naibu Waziri wa Uchukuzi Atupele Mwakibete amesema pamoja na mabehewa hayo mapya Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) inafanya ukarabati mabehewa mengine takribani 30 ya abiria na mabehewa mengine takribani 600 ya mizigo ikiwa ni utekelezaji wa mikakati ya Serikali kuhakikisha mzigo mkubwa unasafirishwa kwa njia ya reli ili kunusuru fedha nyingi zinazotengwa kukarabati miundombinu ya barabara nchini.

“Serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kufanya maboresho makubwa kwenye miundombinu ya reli ikiwemo kuongeza mabehewa ya abiria na mizigo, nina imani mabehewa hayo yakiwasili changamoto ya upungufu wa mabehewa itakuwa imepata ufumbuzi amesema Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete ameitaka TRC kupunguza urasimu kwenye upangaji wa mabehewa ya mizigo ili kuvutia wateja wengi zaidi hasa wanaosafirisha bidhaa mbalimbali kupitia Bandari ya Kigoma na kuelekea Nchi Jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kigoma Ester Mahawe ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu hususani reli kwani kuboreshwa kwake kutainua uchumi wa Mkoa na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa mbalimbali kwa mikoa inayozunguka Ziwa Tanganyika na nchi Jirani.

Kwa upande wake Mratibu wa matengenezo ya njia na Mkuu wa Kitengo cha Usalama na Ulinzi wa reli Mhandisi Ntejo Emmanuel amesema tayari TRC imejiandaa kupokea mabehewa hayo na kipaumbele kitakuwa kwa mikoa yenye idadi kubwa ya abiria na mizigo.

Mhandisi Emmanuel ameongeza kuwa kwa sasa TRC inakamilisha taratibu za manunuzi za kumpata mkandarasi atakafanya maboresho kwenye vituo vya reli na njia kwenye sehemu ya Kaliua hadi Mpanda na Tabora hadi Kigoma ili kuhakikisha walaji wanapata bidhaa kwa wakati.



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akizungumza na Wanafunzi kutoka Chuo Cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) wanaofanya mazoezi kwa vitendo katika stesheni ya reli ya Kigoma, wakati alipotembelea stesheni hiyo Mkoani humo.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akiangalia vipuri vya mabehewa huku Stesheni Masta wa Kigoma Ally Shamte akieleza matumizi yake, wakati Naibu Waziri huyo alipotembelea stesheni hiyo. Mkoani Kigoma.*



# Wami Kuchochea Huduma za Usafiri na Usafirishaji Nchini

Na **Siti Said** - WUU

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, imeonesha dhamira ya wazi katika kuboresha miundombinu mbalimbali nchini hususan ya madaraja ili kurahisisha upatikanaji wa huduma bora za usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara.

Katika kufanikisha hili, ujenzi na uboreshaji wa madaraja katika mikoa mbalimbali nchini umekuwa ukiendelea kutekelezwa na Serikali na hatua mbalimbali zimekua zikionekana kutokana na baadhi ya miradi kukamilika na mingine kuendelea na utekelezaji wake.

Mfano mzuri wa miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa daraja jipya la Wami lililopo mkoani Pwani lenye urefu wa mita 513.5 na barabara unganishi zenye urefu wa kilomita 3.8.

Lengo la kujengwa daraja hili jipya ni kutatua changamoto zitokanazo na daraja la zamani ambalo kwa sasa halikidhi mahitaji ya magari yanayopita kwa kuwa lilijengwa miaka 63 iliyopita (mwaka 1959) na ni jembamba lenye njia moja.

Vilevile barabara zinazounganisha daraja hilo ziko kwenye miinuko mikali na kona mbaya hivyo ajali mbaya na vifo vimekuwa vikitokea mara kwa mara katika eneo la daraja.

**Mradi ulianzaje**

Mradi ulifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwaka 2016 na Kampuni ya International Consultants and Technocrats Pvt Ltd ya India kwa kushirikiana na Apex Engineering Co. Ltd ya Tanzania.

Ilipofika mwezi Oktoba, 2018 Kampuni ya Power Construction Corporation kutoka China ambayo ndio ilipewa dhamana na Serikali ya kujenga mradi huu ilianza kazi rasmi kwa gharama ya shilingi Bilioni 75 huku utekelezaji wake ikiwa ni wa miaka minne na kutarajiwa kukamilika mwezi Novemba 2022.

**Utekelezaji wa mradi ukoje**

Akitoa taarifa ya mradi, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Pwani Eng. Heririsper Mollel, ameeleza kuwa kwa sasa mradi umefika asilimia 86 ambapo kwa upande wa ujenzi wa daraja mkandarasi amekamilisha ujenzi wa sehemu ya chini ya daraja kwa asilimia 100 na sehemu ya juu amekamilisha tabaka la juu la lami mita 256 kati ya mita 513.5 ambayo ni sawa na asilimia 50 ya urefu wa daraja.



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akipitia mpango kazi wa ujenzi wa Daraja jipya la Wami lenye urefu wa mita 513.5 na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 3.8 ambao kwa ujumla ujenzi wake umefikia asilimia 86, mkoani Pwani.*

Ameongeza kuwa kazi nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa makalvati makubwa matatu na madogo saba na uwekaji wa mabomba 188 ya maji kati ya 206 ambayo ni sawa na asilimia 91.

Kuhusu ujenzi wa barabara unganishi Eng. Heririsper amesema kuwa hadi sasa kilometa 3.4 za ujenzi wa tabaka la lami la chini zimekamilika.

**Waziri mwenye dhamana anazungumziaje mradi huu**

Hivi karibuni wakati Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akikagua maendeleo ya mradi huo alisema kuwa Serikali inatarajia kuanza kuruhusu magari kupita juu ya daraja jipya la wami, ifikapo mwezi Septemba mwaka huu.

Akiwa huko, alimuagiza Mkandarasi kukamilisha kazi ndogo ndogo zilizobakia katika daraja hilo ili kurahisisha matumizi salama ya watumiaji wa daraja hilo.

“Hadi sasa kazi zinaendelea vizuri, ni matumaini yangu hadi kufikia tarehe 20 Septemba, mtakuwa mmeshakamilisha kazi zilizobaki ili mimi niweze kuruhusu magari kupita”, alisema Waziri Prof. Mbarawa.

Aidha, Waziri Mbarawa amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha za miradi ya kimkakati ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji nchini.

**Maoni ya Wananchi kuhusu mradi huu**

Mwanaisha Juma: Tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa daraja hili, naamini kukamilika kwake itakuwa mkombozi wa ajali katika eneo hili kwani wengi hupoteza maisha mara kwa mara mahali hapa.

Naye, Hamisi Mwinyiheri, ambaye ni msafirishaji amesema tunatumia muda mwingi kusubiri magari kupita kwa zamu katika eneo hili, tunaamini mradi ukikamilika magari yatapita kwa urahisi kwani hatutasubiriana tena.

Kwa upande wake Fatuma Ramadhani, amepongeza uongozi wa Awamu ya Sita unaoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kufanya kazi nzuri ya kuboresha miundombinu ikiwemo ujenzi wa madaraja makubwa nchini ambapo amesema kuwa licha ya ujenzi huo kurahisisha huduma za usafiri nchini pia hupendezesha miji na majiji.

Kwa ujumla, Serikali bado inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya barabara na madaraja nchini kwani hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 madaraja kama Kiyegeya (Morogoro), daraja la Tanzanite (Dar es salaam), Kitengule (Kagera) na Ruhuhu (Ruvuma) yalikuwa yamekamilika huku ujenzi wa daraja la Wami (Pwani) na JP Magufuli (Kigongo-Busisi : Mwanza) ukiendelea.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**
**Mji wa Serikali Mtumba**
**S.L.P 2888 Ujenzi / S.L.P 638 Uchukuzi**

## DODOMA

**Simu: +255 26 23244455 / +255 26 2322703, 2322702**
**Nukushi: +255 26 2323233 / +255 26 2322704**
**Barua pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwt.go.tz**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

wizarayaujenzinauchukuzi

wizaraUJnaUC

www.mwt.go.tz